
# MUHTASARI

## Uchunguzi wa Haki za Kibinadamu na Utathmini wa Hatari zikumbazo Hifadhi za Jamii Nchini Kenya



Julai 2022

Taasisi ya Utafiti na Sera Mbadala

# Shukrani




**Taasisi ya Utafiti na Mikakati Mbadala ya Sera**
ACK Garden House, 6th Floor
1st Ngong Avenue
P.O. Box 7619-00100
Nairobi, Kenya
www.irpaconsulting.com



**Watafiti wakuu na Waandishi**

- Dr. Ken Nyaundi, Phd.
- Kevin M. Doyle
- Shalom M. Ndiku
- Faith Adu
- Samia Bwana



**Wasaidizi wa Utafiti:**

- David Silakan
- Amina Jillo
- Yoakim Kuraru
- Lucky Tubman



Ingawa utafiti huu uliidhinishwa na The Nature Conservancy, matokeo, uchambuzi, hitimisho na mapendekezo ni jukumu la pekee la IRPA na si lazima yaakisi maoni ya The Nature Conservancy, Kenya Wildlife Conservancies Association, au wahusika wengine.

# Muhtasari

Uzuri wa mazingira ya nchi ya Kenya pamoja na mali asili zake ni utajiri mkubwa wa kitaifa usio na ulinganisho na unaozalisha faida chungu nzima za kijamii na kiuchumi nchini na katika jamii husika.

Hifadhi hizi ni hadithi mwafaka ya historia ya Hifadhi ya Kenya, na matumizi ya kufana ya ardhi katika jamii zinazotoa haki imarishi za asilimali ya utalii wa kimazingira na biashara nyinginezo za Hifadhi. Utafiti mbalimbali wa kimasomo unaonyesha kwamba baadhi ya Hifadhi za kijamii zimeweza kuzalisha matunda mazuri ya Hifadhi ya kijamii na kiuchumi. Kwa vile Hifadhi huunganisha watu pamoja kwa manufaa ya pamoja, huweza kujenga mshikamano na umoja unaochangia kupatikana kwa maadili na mapato ya pamoja. Huu ni uwiano mkubwa wakupendeza kati ya Hifadhi ya wanyama pori na kuheshimu haki za kibinadamu.

Ili kuweza kupata kanuni za pamoja nchini, Hifadhi zote zinapaswa kuimarisha haki za kimsingi za kibinadamu za wanajamii wake. Hata hivyo, madhara ya haki za kibinadamu na athari za kuanzishwa na kuwepo kwa Hifadhi katika jamii bado hazijajulikana kwa uwazi.

Utafiti huu unaangazia hatari za ulinzi, ukuzaji na uangalizi wa haki za kibinadamu katika muktadha wa Hifadhi za kijamii. Unalenga mtazamo wake katika kuangalia hali ya kukuza ufahamu mpana zaidi wa haki za kibinadamu; kujenga taratibu thabiti zitakazowezesha wanajamii watambue, washughulikie na kufuatilia athari zozote mbaya, kadri zinavyojitokeza; na kuanzisha miundo/mbinu inayoweza kutumika, na wanajamii kujifanyia maamuzi yao.

## Matokeo Muhimu

Hii ikiwa Utathmini wa Hatari za Haki za Kibinadamu (THHK) na wala sio Utathmini wa Athari za Haki za Kibinadamu (TAHK), matokeo yanaonyesha madhara makubwa ya uendeshaji wa shughuli na uanzishaji wa Hifadhi kwa lengo la kusisitiza sehemu zinazopaswa kuzingatiwa, huku tukizingatia athari chanya zilizopo na zinazoweza kuwafaidi wananchi wa taifa la Kenya, wanyama pori na mazingira kwa ujumla.

***Usalama wa umiliki wa ardhi na haki za jamii za kutumia, kuimarisha na kuthibiti maeneo na rasilimali zao: Haki kadhaa za kimsingi zimo hatarini kutokana na hatari zinazotokana na umiliki wa ardhi.*** Haki hizi ni haki zinazotokana na Watu wa Kiasili na Jamii za Wenyeji (WKJW au IPLCs), wanawake, chumi za familia/maisha na manufaa yanayotokana na mifano ya Hifadhi zinazoambatana na ardhi. Hatari za ardhi na mazingira zinazoongezeka zinazidisha athari za haki za kijamii na kiuchumi, hasa kutokana na kutegemea ardhi na mazingira kupita kiasi, kwa mapato ya kijamii na kiuchumi ili kuyakimu maisha.

Hifadhi zenyewe pia zimo hatarini hasa pale ambapo umiliki wa ardhi si salama na hali ya matumizi ya rasilimali zake haijashughulikiwa vilivyo. Hali hii inazidishwa na masuala matatu muhimu: (a) Ardhi ya jamii haijadhibitiwa kikamilifu hivyo kuleta hali ya kutoeleweka ya mmiliki wake; (b) Ardhi ya kibinafsi inaweza kushughulikiwa bila matatizo jambo ambalo ni hatari na linaweza kuleta uwezekano wa kuvunjiliwa mbali; na (c) Kuanzisha Hifadhi katika ardhi ya jamii kumaaanisha kuwa uthibiti wa biashara hizi unabakia katika mikono ya serikali.

***Usawa na Uhuru wa Wanawake wa Kutobaguliwa:*** Utafiti huu uligundua uwiano usioweza kutenganishwa kati ya haki za wanawake na za kujumuishwa kijamii na kiuchumi ambazo zinatokana na majukumu ya maisha ya wanawake. Nyingi ya Hifadhi zimo katika jamii ambazo wanaume ndio viongozi na ilionekana kuwa jambo hili huathiri maamuzi yanayofanywa kuhusiana na usawa na uhuru wa kutobaguliwa kwa wanawake. Jambo moja zuri ni kwamba kulingana na Utathmini wa maamuzi katika Hifadhi zilizomo katika mashamba yanayomilikiwa na wanawake yalionekana kuwa ya kiwango cha juu. Hata hivyo, unyanyasaji wa kijinsia unaoripotiwa katika Hifadhi unatoa sifa mbaya, na juhudi zaidi zinapaswa kufanywa ili kuleta mazingira mwafaka ya kulinda kikamilifu haki za wanawake. Kushirikishwa na kuhusishwa kwa wanawake kikamilifu katika maamuzi ni muhimu hasa katika kushughulikia hatari zinazoambatana na haki za kijinsia.

***Ukosefu wa usalama- haki za kuishi, mizozo kati ya binadamu na wanyama, ni tisho kubwa kwa usalama wa mtu na hata mali:*** Ingawa tunafahamu kuwa mizozo ya binadamu na wanyama pamoja na tisho la uhai na mali havisababishwi na kuwepo kwa Hifadhi, malengo ya Hifadhi hizi yamo katika ari zao za kulinda mazingira wakiwemo wanyama. Kutokana na jinsi wanyama wanavyoweza kumdhuru mtu, kumuua au kumharibia mali yake na kumbadilishia mkondo wa maisha yake kabisa; na jinsi serikali inavyochukulia suala zima la kufidia gharama, ni muhimu mno jambo hili lishughulikiwe vilivyo. Kuna nafasi kubwa sana ya kushirikiana na jamii ili kupunguza hasara zilizopo hasa ikichukuliwa kuwa hatari kubwa zaidi inayozikumba Hifadhi ni kuishi pamoja kwa wanyama na binadamu.

***Maamuzi ya Watu Asili na Jamii Wenyeji na haki ya kushiriki:*** Uhusika wa watu asili na jamii wenyeji katika utatuzi wa mizozo, Kuafiki Kwanza bila Shuruti Baada ya Kupewa Taarifa (FPIC), kutoa maamuzi na uamuzi wa kibinafsi ni muhimu katika kupunguza hatari za haki za kibinadamu. Utafiti ulitambua kuwa miundo ya utawala iliyopo katika Hifadhi za jamii kwa sasa, iliyo rasmi au isiyokuwa rasmi, ina uwezo wa kuathiri vibaya kiwango cha maamuzi ya jamii, hivyo basi kuongeza mizozo.

Haki za IPLC zilikuwa katika hatari kubwa zaidi katika jamii tofauti na zile zilizochanganyikana, kwa mfano, Hifadhi ambazo maeneo yake yalivuka mpaka wa kaunti moja na kuingia nyingine na kuwa na makundi tofauti ya watu wanaoishi humo, ama jamii mbili zilizokuwa zikipigana zamani huweza kuzifanya jamii hizi zijiunge

pamoja na kumaliza mizozo kupitia kuanzishwa kwa Hifadhi. Pia, hali za kubaguana ziliripotiwa kutokea kati ya makundi madogo ya watu pale ambapo makundi/kabila kubwa zilionekana kufaidika zaidi na kuthibiti Hifadhi. Watu waliomamlakani au baadhi ya wanajamii hutumia mbinu za vitisho kupunguza haki za makundi ya kijamii hasa makundi madogo na kuyapunguzia uwezo wa kufanya maamuzi ya kibinafsi. Vitisho huathiri haki za matumizi, kufikia maeneo yao ama hata kunufaika kutokana na mapato ya maeneo yao. Mwishowe, hali hii huathiri uwezo wa kujiongoza wenyewe na hivyo kuhatarisha miundo ya tamaduni na hali zao za maisha.

***Faida zinazotokana na Hifadhi:*** Miundo iliyopo ya Hifadhi, hasa ile inayohusisha watu wenye mamlaka ama watu wasio na uwazi na ambao hujigawia sehemu kubwa za ardhi za jamii zao ni tishio kubwa sana katika mgawo wa faida wa Hifadhi za jamii. Nyingi ya Hifadhi zinazomilikiwa na watu wasiojulikana zilionekana kukosa uwazi wa jinsi zinavyopata fedha zake na jinsi mgawo wa faida inayopatikana inavyofikia jamii. Ingawa ilidhaniwa kuwa nyingi ya fikra na maoni ya wanajamii waliohusishwa katika utafiti yalikuwa ya hatari, baadhi ya fikra hizi, hasa za ufisadi zilionekana kuwa za msingi. Katika Hifadhi zote, mpya na zilizoimarika, baadhi ya wadau walilalamikia hali ya kutokuwa na uwazi wa jinsi Hifadhi hizo zinavyozalisha faida zao za kifedha.

## Mapendekezo

Ili kuimarisha utambuzi wa kiwango cha juu cha masuala na hatari zinazoambatana na haki za kibinadamu, kutengeneza utaratibu unaoziwezesha jamii kuendelea kujitambua, kushughulikia na kufuatilia ukiukaji wowote wa haki za kibinadamu na athari zake, na kujenga miundo inayoweza kutumiwa, tunapendekeza yafuatayo:

a. Serikali ya Kitaifa na zile za kaunti, Hifadhi na mamlaka nyingine za udhibiti ziwe na: Uwezo wa kuharakisha utoaji wa vyeti vya mashamba kwa haraka kupitia Tume ya Kitaifa ya Ardhi ili kuhakikisha usalama wa kumiliki ardhi ya kijamii; Kuhakikisha kuna mazingira bora yanayowezesha ukuaji wa Hifadhi za kijamii kupitia kuoainisha ukinzano uliopo wa sera na sheria zinazoongoza uratibu na usimamizi wa rasilimali za serikali zinazosimamiwa na mawakala wake; Uimarishaji wa utendakazi wa wadau, na wanaosimamia haki waweze kuwa na vikao vya mara kwa mara vya ukaguzi wa haki za kibinadamu vinavyoshirikisha wadau wote; na, Kutambua, kuchunguza na kudumisha utamaduni au njia mbadala za utaratibu wa kutatua mizozo hasa ile inayohusiana na usimamizi wa mali asili.

b. Sekta ya kibinafsi inaweza kuchukua jukumu muhimu la kuimarisha utenda kazi wa jamii mbalimbali wa kusimamia Hifadhi zao kupitia: Kuwa waangalifu wanaposhughulikia maombi ya FPIC na ujumuishi kabla ya kutoa fedha za ruzuku za kuanzisha Hifadhi mpya au kusaidia zile zilizopo; Kusisitiza kuwepo kwa utafiti msingi kabla ya kuanzishwa kwa Hifadhi ili kukuza haki za jamii za FPIC na kukubaliwa na wenyeji; na, Kusaidia kuandika kumbotabaka za masomo (training modules) ambazo zinaweza kutumika katika Hifadhi kujenga utendakazi wa usimamizi na uimarishaji wa mashirika yao, shughuli, hati za sera na mikakati ya kijamii, kiuchumi na kimazingira.

c. Hifadhi za kijamii zaweza kuweka kipaumbele mikakati tofauti inayoweza kuleta faida kubwa kwa wanajamii pamoja na ulinzi wa maadili ya viumbe hai yanayojumuisha: Kubuni na kutekeleza mikakati inayolenga kuimarisha na kujumuisha ushiriki wa jamii katika mipango ya Hifadhi ili kudhibiti haki zao za kushiriki katika kujifanyia maamuzi; Kutambua na kupunguza vikwazo vinavyozuia ushiriki wa pamoja, kuongeza uwakilishi wa wanawake katika halmashauri/bodi na kuwa na miundo ya maisha inayoweza kujisimamia inayowapa uwezo wanawake kiuchumi; na ushirikiano wa makundi madogo ya watu pamoja na wanajamii wa kuweka mikakati ya kitamaduni ya kutatua mizozo, kusambaza habari kuhusu mikakati hiyo na kuhakikisha kwamba kanuni zilizowekwa zinafuatwa kikamilifu ili kuwaridhisha waliokosewa.

Kutokana na mitazamo hii, ripoti inatoa hitimisho zifuatazo:

- Utambuzi mpana wa masuala na hatari zinazohusiana na haki za kibinadamu: Kiwango cha ufahamu kati ya watu asili na wenyeji na askari mwitu kilikuwa cha chini sana wakati wa kukusanya takwimu. Hakukuwa na maingiliano yenye mtazamo wa haki za kibinadamu kati ta wadau wengi na wamiliki haki. Shughuli hii ilikuwa ya mafunzo makubwa kwao na walionyesha hamu kubwa ya kutaka kuelewa haki hizo na jinsi zinavyohusiana na kazi zao za kila siku.

- Mikakati ya jamii ya kuendelea kutambua, kushughulikia na kufuatilia ukiukaji wowote wa haki za kibinadamu na athari zinazoweza kutokea: Utafiti huu haukupata ushahidi wa kutosha wa mikakati iliyowekwa ya kufuatilia athari za haki za kibinadamu ambazo zinawezesha kutambua mitindo, misururu na suluhisho ya kushughulikia ukiukaji wa haki za kibinadamu.

- Miundo ambayo jamii inaweza kutumia kuendeleza maamuzi yao kibinafsi: Kwa kiasi fulani, kuna miundo kadhaa ambayo jamii zinaweza kutumia kukuza maamuzi yao ya kibinafsi, iwe ni serikali za kaunti, Wizara ya Ardhi, Tume ya Ardhi ya Kitaifa, Tume ya Haki za Kibinadamu ya Kenya na Tume ya Kitaifa ya Haki za Kibinadamu. Pia, miungano ya kimaeneo ya Hifadhi za wanyama na KWCA zinapaswa kuwa wazi katika majukumu yao ili kuhakikisha kuwa jamii ambazo ama tayari ni washiriki katika Hifadhi fulani au wametambuliwa kushiriki katika Hifadhi mpya, wanapewa nafasi na uwezo wa kujiamulia.

